**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI**

**YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**

**SHULE YA SEKONDARI RUNGWA**

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO 2024**

S.L.P 504,

Namba za simu MPANDA

Mkuu wa Shule 0766989885/0782358113 18/04/2024

Makamu Mkuu wa Shule 0766736770

Mlezi wa wanafunzi 0762532970

Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi ………………………………..,

S.L.P ………………………,

…………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI RUNGWA, HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA – MKOA WA KATAVI 2024**

1. Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii mwaka 2024 katika tahasusi ya …………...
2. Shule ni ya bweni kwa wavulana wa kidato cha tano na sita, ipo umbali wa kilomita nne (4) kutoka katikati ya Manispaa ya Mpanda, wilaya ya Mpanda, mkoa wa Katavi. Usafiri wa bajaji, bodaboda na taxi unapatikana katika standi kuu na stesheni ya treni hadi shuleni kwa bei nafuu.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza rasmi tarehe **01/07/2024.** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **01/07/2024** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **15/07/2024.**

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 Sare za shule**

a) Suruali mbili nyeusi (kitambaa aina ya esteem namba 2, mshono umeambatanishwa)
b) Shati mbili nyeupe za pamba zenye mikono mirefu zisizo na urembo wowote zenye mfuko mmoja juu kushoto.

c) Masweta mawili rangi ya kijani kibichi
d) Tai mbili nyeusi ndefu zilizoshonwa kwa kutumia aina ya kitambaa cha suruali
e) Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba vyenye kisigino kifupi (jozi mbili).
f) Soksi fupi nyeupe angalau jozi mbili
g) Mkanda mweusi wa kuvalia suruali
h) Suruali mbili za kushindia (shamba dress) rangi ya kahawia (rejea kiambata cha mshono wa suruari)
i) Fulana yenye nembo ya shule inapatikana shuleni
j) Track suit jozi moja rangi ya kijani, bukta, raba na fulana ya kijani isiyo na maandishi kwa ajili ya michezo

   **NB: mwanafunzi haruhusiwi kuja na mavazi aina yoyote ile zaidi ya sare zilizotajwa hapo juu.**

**2.2 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni;**

i. Ream ya karatasi moja ( kila muhula)
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)
iii. Scientific calculator ( kwa wanafunzi wa masomo ya hisabati)
iv. Madaftari makubwa yasiyopungua matano
v. Mkebe wa hesabu moja, Kalamu, penseli na rula
vi. Dissecting kits (kwa watakaosoma biology)
vii. Dissecting tray 1(kwa watakaosoma biology)
viii. Godoro dogo la size 2½x6
ix. Mashuka jozi mbili rangi ya samawati (bluu bahari)
x. Mto na Foronya rangi ya samawati (blue bahari)
xi. Chandarua (01) rangi ya samawati (bluu bahari) – (pembe nne)
xii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe
xiii. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
xiv. Mfagio 1 wa ndani (soft groom)
xv. Mopper kwa ajili ya kukaushia maji
xvi. Mfagio mkubwa moja kwa ajili ya usafi wa nje
xvii. Jembe moja na mpini wake

**Michango ya Shule**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

**Michango yote ya shule ilipwe benki katika akaunti namba 61901100051 iitwayo Rungwa secondary school revenue collection account katika tawi au wakala wa NMB popote Tanzania NYUMA YA BENKI PAY IN SLIP UANDIKWE MCHANGANUO WA MALIPO HUSIKA. HAKUNA MWANAFUNZI ATAKAYEPOKELEWA BILA BANK PAY IN SLIP (NAKALA YA STAKABADHI YA MALIPO YA BENKI)**

**2.3 Matibabu ya Mwanafunzi**

Gharama za matibabu kwa mwanafunzi atakapokuwa shuleni ni jukumu la mzazi. Ili kupunguza gharama na usumbufu mwanafunzi anatakiwa kuja na kitambulisho cha Bima ya afya (NHIF). Kwa wale ambao hawana kitambulisho hicho mwanafunzi aje na shilingi 50,400/= ili aweze kutengenezewa.

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu pamoja na sheria ndogondogo za shule. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

### 3.1. Sheria na kanuni muhimu za shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
vi. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
vii. Kutunza mali za umma
viii. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye incha kali na dawa bila idhini ya daktari
ix. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini au kumshawishi mwenzie kubadili dini wawapo shuleni

MUHIMU:

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi
- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni allilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi bweni ambalo hajapangiwa. Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja tu
- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa shule (msiba au Ugonjwa)

3.2 **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule**;

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule
vii. Kufuga ndevu

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya
ix. Uvutaji wa sigara
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa
xi. Ubakaji
xii. Kusababisha mimba
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xiv. Kuingia kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni
xv. Kumiliki au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xvi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
xvii. Kudharau bendera ya Taifa
xviii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu

Viambata na Fomu Muhimu

a) Fomu ya kupima afya ambayo inatakiwa kujazwa na daktari anayetambuliwa kisheria
b) Fomu ya historia ya wazazi na mwanafunzi
c) Fomu ya mzazi na mwanafunzi kukiri kukubalina na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayoyolewa na shule
d) Picha nne (4) za wazazi/walezi au ndugu watakaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamaoja na namba zao za simu

**5. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO/ MAAGIZO HAYO NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU**

*Karibu sana Rungwa Sekondari*

Mwl Emmanuel C Mwamwezi
Mkuu wa Shule

KIAMBATA 'A'

ORODHA YA VITABU MBALIMBALI VYA MASOMO

GEOGRAPHY

1. (Colin Buckle), LANDFORMS IN AFRICA
2. C.R. KOTHARI), RESEARCH METHODOLOGY
3. (H.C. TRURAN), A PRACTICAL GUIDE TO STATISTICAL MAPS AND DIAGRAMS 4. (Goh cheng Leong.Gillian.C. Morgan), HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY
5. (DAVID WAUGH), GEOGRAPHY-AN INTIGRATED APPROACH.
6. (JOHN.M. PRITCHARD), PRACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA 7. (R.B. BUNETTE), PHYSICAL GEOGRAPHY IN DIAGRAMS FOR AFRICA.
8. Geography for Secondary Schools form Five (TIE)
9. Geography for Secondary Schools Form six (TIE)

HISTORY PAPER ONE

1. Hallert, R. (1983). Africa Since 1875 Vol.3. East African Educational Publishers. Nairobi, Kenya.
2. July, R.W. (1992). A History of the African People, East African Educational Publishers, Nairobi, Kenya.
3. Illife, J. (1995). Africans, the History of the Continent. Edinburg, Cambridge; University Press, London UK.
4. Manning, P. (1990). Slavery and African Life; Occidental Oriental and African Slave trade, Cambridge University Press.
5. Njiro, E. (1989). A History of Africa in the 19th century. Literature Bureau Nairobi, Kenya.
6. Rodney, W. (1976). How Europe underdeveloped Africa, Publishing House, Dar es salaam, Tanzania.
7. Shillington, K. (2004). History of Africa. MacMillan Publishers. Hong Kong, Japan.
8. Davidson, E. ef al (1997); The growth of the African civilization East and Central Africa to the late 19th century, Longman Group Limited, Singapore.
9. Freud, B. (1998): The making of contemporary Africa; The Development of African societies since 1800, Colorado, Lynne Rienner Publishers.
10. Kimambo, I and Temu, A (1969); A History of Tanzania, East Africa Publishing House Nairobi, Kenya.
11. Robin, H. (1993); African since 1875 A modern History, East African Publishers Ltd., Nairobi, Kenya.
12. Roland, O. and Anthony, A. (2007). Africa since 1800, Cambridge University Press, New York, USA.
13. History for Secondary Schools Form five (Tanzania Institute of Education)
14. History for Secondary Schools Form Six (Tanzania Institute of Education)
15. History for secondary schools: Form Five (TIE)
16. History for Secondary Schools: Form Six (TIE)

HISTORY TWO

1. Nelson throne Essential modern world history
2. History of 21st century (World history) (Oxford)
3. H.L. Peacock. A History of Modern Europe 1789-1981 seventh Edition (2010) 4. The History of Modern World (2007) 6th Edition by Oxford University Press.

GENERAL STUDIES

1. Richard, R.F. Mbalase. General Studies For Advanced Level Certificate;
2. Mgaywa, B.M. General Studies for Advanced level 3rd Ed.
3. Joannes Bigirwa Mungu & Sospeter.M. Deogratias. Understanding Advanced Level General Studies for Advanced Secondary School Education;

BASIC APPLIED MATHEMATICS & ADVANCED MATHEMATICS

1. Basic Applied Mathematics for Secondary School.
2. Basic Applied Mathematics Review.
3. Basic Applied Mathematics (TIE)
4. Advanced Mathematics book one and two by Backhouse
5. Advanced Mathematics book one and two by Chand
6. Advanced Mathematics by Shayo

ECONOMICS

1. Ambilikile C.M (2010) Economics for Advanced level. (Part I & II)
2. MUDIDA, R. (2003), Modern Economics 1st Ed. Nairobi Kenya.
3. Basic Economics: Tayebwa Mugisha Bernard 5th edition 2011
4. Principles of Economics: Jinghang
5. Basic Economics for East Africa: Dhumba Sentamu
6. Model Questions and Answers: Tayebwa Mugisha Bernard 7. Modern Economics Theory Dr. K.K Dewell and Navalur
8. Principles of Economics: D.N. Dwived 2nd edition.

BIOLOGY

1. Advanced Biology: Michael Kenti (2000) 2nd edition
2. Biological Science: Taylor et al 2010
3. Understanding Biology; Glenn and Toole, G (1999)
4. Advanced Biology Review (2000 -2016)

CHEMISTRY

1. S. Chand Conceptual Chemistry for Class XI and XII
2. Tanzania Institute of Education, Advanced level Inorganic Chemistry part I and II
3. Advanced Chemistry Review (2000 – 2012)

ENGLISH

1. Francis Mnyani (2014). Contemporary English for A. Level (V &VI)
2. Nicholous Ashery (2010). English Practical Approach for Advance level
3. Michael Kadeghe (2010). The Real English textbook for A level (V & VI)
4. TIE (2016/2017). English Language for Secondary School for Advanced level

Reading Books

1. Ayi Kwel Armah, the beautiful one are not born
2. Chinuo Achebe – Man of the People

3. Chinuo Achebe – His Excellence the Head of State

Plays
Heinrich Iblem – An enemy of the people

**KIAMBATA “B”**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**

**SHULE YA SEKONDARI YA RUNGWA**

**Kumbukumbu Namba: RSS/SA/2021/…………**

**HISTORIA YA WAZAZI NA MTOTO ALIYECHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII:-**

A. WAZAZI/WALEZI

1. Jina la Baba ………………………………………………….. Hai/Si hai

2. Jina la Mama ……………………………………………….. Hai/ Si hai

3. Kama Baba si hai jina la mlezi ni ………………………………………………………….

4. Kazi/Shughuli ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………….

5. Anwani ya

Mzazi/Mlezi………………………………………………………………………………...

6. Uraia wa wazazi

-Baba Mtanzania/Si Mtanzani

-Mama Mtanzania/ Si Mtanzania

7. Wakati wa likizo mtoto/Mwanafunzi unataka aende wapi?

……………………………………………………………………………………………………

8. Jina la mtu aendako ……………………………………………………………………..

Uhusiano na mtoto/mwanafunzi.

………………………………………. ………………………………………………………..

SAHIHI YA BABA/MLEZI WA MWANAFUNZI

TAREHE …………………. TAREHE ………………………….

**KIAMBATA ‘C’**

RUNGWA SECONDARY SCHOOL

FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical officer in respect to all form of entrants

Student’s full name ………………………………………………………………………………..

Age ……………………………………… Years ……………………….. Sex …………………...

Blood count (red and whites) …………………………………………………………………………

Stool examination ……………………………………………………………………………….

Urine analysis………………………………………………………………………………………

Syphilis and other venereal diseases test …………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………

T.B test ……………………………………………………………………………………..

Eye Test ……………………………………………………………………………………………

Ears ………………………………………………………………………………………………...

Abdomen …………………………………………………………………………………………...

Urine for plant test ……………………………………………………………………………

Test for pregnancy ……………………………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION
Defects, impotents (e.g. arms, legs etc) infections, chronic or family diseases etc

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

I certify that the named above is fit to pursue further studies

Station …………………............ Signature …………………………………

Date. ………………….. … Designation……………………………….

KIAMBATA 'D'

# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA
# SHULE YA SEKONDARI RUNGWA

Kumbukumbu Na………………………………

Mkuu wa Shule, sekondari
ya Rungwa,
S.L.P 504,
Mpanda

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mimi ………………………………………………………………… nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuwa kuchaguliwa kwangu kuingia shule ya Sekondari ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu ni chache. Hivyo nakubali kujiunga na shule ya sekondari ya Rungwa. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule. Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu kweli daima.

Nitalinda hadhi/heshima ya Shule ya Sekondari ya Rungwa na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

Tarehe …………………………. Sahihi ya mwanafunzi ………………………………

Mimi Mzazi/ Mlezi …………………………………………. Nimeshuhudia mtoto wangu ………………………………………. akikubali kwa hiari kujiunga na shule hiyo ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kumlea mtoto wangu naamini tutakuwa tunawasiliana.

Tarehe ………………………………Sahihi ya Mzazi/Mlezi……………………………………